International Journal of
**Linguistics**
*(IJL)*

# MATUMIZI YA LUGHA KATIKA MIMU (*MEMES*) KWENYE MITANDAO YA KIJAMII NCHINI KENYA

Anne Wangari Munuku




IPRJB
INTERNATIONAL PEER REVIEWED JOURNAL AND BOOK PUBLISHING

International Journal of Linguistics

ISSN 2710-4788 (online)

Vol.3, Issue 1. No.3. pp 30 - 49, 2022

www.iprjb.org

# MATUMIZI YA LUGHA KATIKA MIMU (*MEMES*) KWENYE MITANDAO YA KIJAMII NCHINI KENYA

Anne Wangari Munuku

Chuo Kikuu cha KCA, Kenya

Barua Pepe: amunuku@yahoo.com

**Iksiri**

Makala hii imeangazia lugha ya mawasiliano katika utanzu mpya wa mimu ambao ni aina ya fasihi kidijitali katika mitandao ya kijamii ya Facebook na WhatsApp nchini Kenya. Matlaba ya makala hii ni kufafanua utanzu huu katika muktadha wa matumizi ya lugha nchini Kenya. Uundaji mimu ni jambo ambalo limeanza kufanyika kwa wingi katika mitandao ya Kijamii na kwa hivyo kuna haja ya kulifanyia utafiti. Makala hii ina malengo matatu: kutoa mifano ya jumbe za mimu zinazoundwa na Wakenya katika mitandao ya Facebook na Whatsapp; kubainisha sifa za jumbe hizo kimuundo na kimtindo; na kuchunguza dhima ya utanzu wa mimu katika jamii. Mbinu ya utafiti iliyotumika katika kazi hii ni usanifu taaradhi na data ilichanganuliwa kwa kutumia Uchanganuzi maudhui ambapo data ilitambulishwa kwa kuiweka katika kategoria maalum. Mimu 51 zilizorejerelewa katika makala hii zilikusanywa kupitia kwa makundi ya Whatsapp anayoshiriki mwandishi na katika kurasa za Facebook za mtafiti na 'marafiki' wake wa mtandaoni pamoja na kurasa za wasanii mashuhuri wa mimu. Mimu zilizorejelewa katika makala hii ziliundwa kati ya mwaka 2017 na 2021.Mimu hizo zimechanganuliwa kiisimu kwa kurejelea mawazo ya nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Kilongo ya Fairclough (1995). Nadharia hii imeafiki Uchanganuzi wa data husika na imefaulu katika kudhihirisha sifa na miundo ya mimu. Matokeo ya utafiti huu yanadhihirisha kuwa mimu zinazoundwa na Wakenya huwa na dhima maalum katika jamii na pia huwa na sifa za kipekee kimuundo, kimsamiati, kisemantiki na kipragmatiki.

**Istilahi kuu**: *Mimu, Usemi, Matini, Uchanganuzi Hakiki wa Kilongo, Diskosi*

International Journal of Linguistics

ISSN 2710-4788 (online)

Vol.3, Issue 1. No.3. pp 30 - 49, 2022

www.iprjb.org

## UTANGULIZI

Teknolojia ya habari na mawasiliano imeathiri sekta nyingi nchini Kenya na kwingineko duniani. Kuingia kwa mitandao ya kijamii kuanzia mwaka wa 2004 na kuendelea kumechangia pakubwa katika kupanua nafasi ya demokrasia kwa wanajamii kimawasiliano. Kupitia kwa mabadiliko haya, hasa yale ya uanahabari dijitali na uanahabari-raia, watu wasio na mafunzo rasmi ya uanahabari na mawasiliano ya umma sasa wamepata nafasi ya kutoa maoni, mawazo na kuburudishana mtandaoni. Aidha, Wakenya wamepata nafasi sio tu ya kuburudishana bali pia kupinga masuala ya kisiasa, kubainisha hasira na kujenga ushirikiano wa pamoja katika kupinga sera mbovu za kiutawala kwa njia ya utani wa mtandaoni (Mukhongo, 2020) Hali hii mpya ya mawasiliano imewapa raia wa kawaida nafasi ya kujieleza, kukosoa na hata kuungana na wengine katika ujenzi wa jamii ya mtandaoni. Matumizi ya mimu katika mitandao ya kijamii hutumika kuendeleza kinaya na ucheshi (Rasheed, 2020; Kulkarni, 2017).

Makala hii inanuia kueleza sifa za utanzu wa kiutani ambao hutumika katika mitandao ya Facebook na Whatsapp.  Aidha, matumizi ya lugha katika mimu hizi pamoja na jinsi lugha tofauti zinavyotumika kuziunda yanaangaziwa. Kenya ni nchi yenye mtagusano wa lugha nyingi kwa kuwa ina wingi-lugha. Katika mawasiliano yao ya kawaida, Wakenya huchanganya lugha na mimu wanazounda zinazoonekana kufuata mtindo huu. Matumizi ya lugha mbili au zaidi katika mimu moja ni suala linaloangaziwa katika uchanganuzi wa mimu hizi. Mimu zinachukuliwa hapa kama aina maalum ya diskosi ya mtandaoni inayofaa kufanyiwa uchunguzi ili ieleweke vizuri zaidi. Iloh (2021) Kwa jumla, makala hii itazungumzia sifa za mimu hizo kama diskosi katika mitandao ya kijamii iliyoteuliwa. Diskosi katika matini hii ni jumbe za mimu katika mitandao ya kijamii ya Whatsapp na Facebook ambazo huchukua muundo wa vichekesho na hujulikana kama "*memes*" na "*gafes*" kwa lugha ya Kiingereza. Katika makala hii neno *mimu* linatumika baada ya kutoholewa kutoka kwa neno la Kiingereza *memes*. Malengo ya makala hii ni: kutoa mifano ya jumbe za mimu zilizoundwa na Wakenya katika mitandao ya kijamii ya Facebook na Whatsapp; kubainisha sifa za kiisimu za mimu hizo; na kuchunguza dhima za mimu hizo katika jamii. Mimu zinazorejelewa katika makala hii zilikusanywa kupitia kwa makundi ya Whatsapp anayoshiriki mtafiti na katika kurasa za Facebook pamoja na kurasa za wasanii mashuhuri ambazo ziko wazi kwa matumizi ya umma.

### Taarifa ya Tatizo la Utafiti

Uundaji mimu ni jambo ambalo limezua ubunifu wa kipekee mtandaoni. Mimu huundwa na watu kutoka takribani maeneo yote ulimwenguni. Ubunifu huu unastahili kufanyiwa utafiti ili ueleweke kisifa, kimuundo na kimatumizi. Kwa kuwa jamii huwa katika viwango tofauti kimaendeleo ni muhimu kujikita katika utafiti wa utanzu huu katika jamii mahsusi. Mimu zimeibuka kuwa njia ya kawaida ya mawasiliano ya kila siku na husheheni sifa za kitamaduni za jamii husika zinazopaswa kuchunguzwa na watafiti. Mimu hubadilika haraka kupitia kwa ubunifu na pia hudhirisha sifa anuai kama vile michoro, picha, video au changanyiko wa sifa za sikizi-oni na kwa hivyo ni muhimu kuzichanganua ili ziendelee kueleweka. Utafiti wa utanzu huu utachangia pakubwa utafiti wa sayansi za kijamii hasa fasihi na mawasiliano kwa jumla. Mimu zinazorejelewa katika makala hii ni za mtandaoni pekee na ambazo zinahusishwa na wasanii na raia wa Kenya. Tafiti

zilizofanywa kuhusu utanzu huu nchini Kenya zimegusia masuala maalum kama vile matumizi ya mimu kukosoa serikali tawala wakati wa janga la Ugonjwa wa Virusi vya Korona wa 2019 (UVIKO-19) uliofanywa na Nabea (2021); na Uchanganuzi wa mimu za kisiasa zinazotumia utani kupinga sera mbovu na kuwapa raia wa kawaida sauti kuhusiana na masuala ya utawala, uliofanywa na Mukhongo (2020). Makala hii inaangazia sifa na dhima za mimu katika jamii ya Wakenya kwa jumla na jinsi masuala ya Kijamii huchangia kuibuka kwa mimu hizi mtandaoni. Aidha, makala hii inanuia kuongeza maarifa katika usomi wa diskosi na kufungua mjadala kuhusu utanzu mpya wa fasihi ya kidijitali unaokua haraka katika mitandao ya kijamii.

## MAPITIO YA MAANDISHI

Matumizi ya mimu katika mawasiliano yamekuwepo kwa muda lakini katika miaka ya hivi karibuni jamii nyingi zimeanza kutumia mimu kuwasilisha dhana na jumbe tofauti mtandaoni kwa mapana zaidi. Kulingana na Leong (2015) katika Kulkarni (2017), mimu zilianza zamani hasa kwa kurejelea zile zilizotumika kama nyenzo za kusambaza propaganda wakati wa vita vya kwanza vya dunia kupitia kwa picha na matini za kuendeleza bezo pamoja na michoro ya kisanii. Kwa kuwa mimu huhusisha ubunifu wa kisanii na ujuzi wa stadi za kiteknolojia, mimu zinaweza kuchukuliwa kama utanzu wa sanaa ya fasihi kidijitali unaotumika katika mtandao. Mimu huundwa kwa kutumia mkusanyiko wa maneno, sauti, video, michoro na picha. Vilevile, mimu huweza kueleweka kama aina ya utani au ujumbe unaotokana na uvumi au habari halisi kuhusu suala muhimu katika jamii na unaosambazwa kwa njia za kidijitali. Flecha na wengine (2021) wanaeleza mimu kama njia ya kuwasilisha vipengele na jumbe za kiutamaduni kwa namna inayosambaa haraka na kwamba mimu huweza kuelekeza matendo na fikra za jamii mahsusi. Kadhalika, Flencha na wenzake (weshatajwa) wanafafanua kuwa mimu ni muhimu kwa kuwa kupitia kwa mitandao ya kijamii watu hushiriki katika ujenzi wa maisha ya kijamii wanapobadilishana maoni, ujuzi, fikra na hisia zinazotokana na tajriba zao na ambazo hujenga matini za mimu mbalimbali. Usambazaji wa mimu hufanywa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine kupitia kwa barua meme, blogu, jumbe fupi na mitandao ya kijamii kama vile *Facebook, WhatsApp, Instagram* na *You Tube.*

Asili ya mimu inaweza kuhusishwa na mawazo ya mwanabayolojia Richard Dawkins katika kitabu chake *The Selfish Gene* kilichochapishwa mwaka wa 1976 (Iloh, 2021). Dawkins alizungumzia jinsi vipengele vya utamaduni vinavyoenezwa na kuzalishwa katika jamii fulani kisha kusambazwa miongoni mwa jamii tofauti. Kulingana naye, msanii anapounda mimu huwa anachukua wazo lolote la kijamii na kuligeuza kwa kulipa sifa mpya kisha akalisambaza kwa njia maalum. Hali hii inaweza kuhusishwa na jinsi mwanasayansi Charles Darwin alivyofafanua dhana ya ubadilikaji wa misimbojini ya kibayolojia. Hata hivyo, Iloh (2021) anaeleza kuwa badala ya mimu kubadilika na kusambaa kama msimbojini aliozungumzia Darwin, mimu hubadilishwa kimaksudi na binadamu kupitia kwa ubunifu. Mabadiliko ya maudhui na miundo ya mimu huambatana na mabadiliko katika maisha ya jamii husika. Kwa sababu hii ni muhimu kufanya utafiti wa utanzu huu wa mimu ili kubainisha sifa zinazoibuka hususan katika enzi hii ya utandawazi.

Dhana ya mimu za mtandaoni ilizungumziwa kwa mara ya kwanza na Mike Godwin katika jarida la *Wired* mnamo mwezi Juni 1993. Kwa hakika kuunganisha matini na picha hakumaanishi kuwa mtu ameunda mimu. Badala yake, Iloh (2021) anasisitiza kuwa njia ya kuwasilisha na kasi ya mawasiliano hayo ndizo huifanya mimu kuitwa mimu. Kwa hivyo mimu ni utanzu wa mtandaoni uanotegemea usambazaji wa kasi pamoja na kuwa mtandao huwezesha mawasiliano mapana ya wanajamii anuai. Dhana ya mimu imebadilika kimatumizi katika mpito wa wakati ikilinganishwa na jinsi ilivyotumika awali. Katika enzi ya sasa mimu, hususan katika vyombo vya habari, hurejelea utanzu wa mawasiliano ambao hukuzwa na kusambazwa na washiriki tofauti kwenye mitandao ya kijamii (Milner, 2012).

Mabadiliko makubwa yamekuwa yakifanyika katika sekta ya mawasiliano ya umma tangu kuingia kwa teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA). Ni vigumu katika enzi hii kuweka mipaka kati ya wale wanaoibuka na habari na wale wanaotumia/kupokea habari hizo. Hadhira katika mtandao huweza kuwa waibuaji habari na vilevile wapokezi wa habari. Vyombo vipya vya habari vimewezesha mabadiliko mengi kufanyika kwenye mtandao ikiwemo kuzuka kwa fasihi kidijitali. Kulingana na Henry (2019) vyombo vipya vya habari vinaweza kutambulishwa kupitia kwa vipengele kama vile udijitali au matumizi ya teknolojia ya mtandao, mwingiliano wa watumiaji ambao huonekana kubadilishana nafasi, mwingiliano wa matini, mwingiliano wa mitandao, ufikiaji na utumiaji wa mitandao na uwezo wa kubadilika panapo haja. Kama utanzu unaotumia vyombo hivi vipya, mimu hudhihirisha sifa hizi zote kimatumizi pamoja na kwamba huwa zinaundwa kwa kutumia zanatepe za mtandoni.

Baukhage (2011) anasema baada ya mimu kuundwa huwa zinasambazwa kupitia kwa mitandao ya kijamii, blogu, barua meme, tovuti na jumbe fupi. Uundaji wa mimu huweza kujumuisha maneno ya kuvutia yanayojitokeza kama virai, picha na hata video. Mimu huenezwa kwa kutolewa maoni, kuigwa na kuzalishwa kwa kurejelea mada au habari zinazohusiana na mimu asilia. Mimu husambaa kwa haraka mtandaoni kupitia kwa injini pekuzi kama *Google* na *Twitter* zinazowawezesha watumiaji wa mtandao kupekua, kupakia na kupakua mimu zozote wanazovutiwa nazo. Kwa mfano, mtumiaji wa mtandao anapopokea mimu, kwenye mtandao wa *Facebook* anaweza kuzisambaza kupitia kwa mitandao ya *WhatsApp* na *Instagram* na hivyo kuwafikia watu wengi kwa muda mfupi. Aghalabu mawasiliano haya hutekelezwa kupitia kwa simu za mkononi ambazo sasa zinamilikiwa na idadi kubwa ya watu duniani. Mathalani, nchini Kenya kuna watumiaji wa simu zaidi ya milioni hamsini na tano kulingana na ripoti ya Mamlaka ya Mawasiliano-kenya ya mwaka 2020. Jambo hili linamaanisha kuwa asilimia kubwa ya Wakenya inaweza kutumia huduma za mtandao almuradi wanamiliki simu janja.

Jenkins (2006) anasema mimu huweza kuchukuliwa kama mojawapo wa tanzu zinazotumika katika vyombo vya utangazaji ambapo kuna mwingiliano na mabadilishano ya kiwango kikubwa kati ya mtoaji habari na hadhira (*participatory media)*. Mimu hubadilika kimuundo na kupata sura mpya pindi tu inapoanza kusambazwa kwa watumiaji wengi. Kila mara mimu inapobadilika, dhana mpya huzuka na jambo lililokuwa likijadiliwa huanza kueleweka upya (Milner, 2012). Mimu hutumia picha na maneno kufanya utani unaojikita katika masuala mazito ya kijamii. Waundaji wa mimu mitandaoni hutumia zanaviolwa maalum kwenye mtandao kuunganisha picha, maneno, michoro na sauti au kuandika tu ujumbe unaodhihirisha ubunifu wa kisanaa kupitisha

ujumbe maalum. Mtu yeyote mwenye simu janja anaweza kuunda mimu bora tu ana uwezo wa kutumia programu-tumizi na zanaviolwa zinazofaa kuunda mimu fulani

Nafasi ya vyombo vipya vya habari katika uundaji na usambazaji wa mimu ilidhihirika zaidi kuanzia miaka ya tisini na kufikia sasa mimu zimeibuka kuwa utanzu unaotambulikana kama nyenzo ya mawasiliano kote ulimwenguni. Mitandao tofauti ya kijamii ilipozuka miaka ya 2000 mimu zilianza kuundwa na zikakua haraka kimatumizi. Kwa mfano, mtandao wa video wa *You Tube* ulipoanza kutumika mwaka wa 2005, mimu zilizotumia sauti na picha, ambazo hujulikana kama mimu za sikizi-oni (*audio-visual*), ziliibuka. Nyingi za mimu hizi huwa video fupi fupi zinazolenga kuwasilisha wazo moja la kijamii kama vile udanganyifu wa wanasiasa, hali ya anga, hali ngumu ya maisha na kadhalika. Mitandao ya *Facebook* na *Twitter* ilipoingia mwaka wa 2004 na 2006 mtawalia, mimu ziliendelea kutumika kwa wingi hasa baada ya zanaviolwa maalum zilizowaruhusu watumiaji kuunda mimu, kuundwa mtandaoni. Hata hivyo, Wakenya walishiriki katika uundaji wa mimu kwenye mitandao hii ya kijamii kuanzia mwaka wa 2010 wakati mimu za kwanza zilizohusu mhusika Makmende ziliundwa (Ekdale na Tully, 2014).

Milner (keshatajwa) anasema mimu zinaweza kuchukuliwa kama matini za kijamii kwa maana ni mali ya jamii na huzungumzia masuala ya kijamii. Mimu kama matini za kijamii huwa na sifa ya kisanii ambapo washiriki wenye ujuzi maalum wa kitamaduni hutumia ustadi wao kueleza na kubainisha uhalisia wa maisha yao. Aidha, matini za kijamii ni rasilimali ya jamii. Matini za kijamii hutumika kubainisha uneni tendi, uasilia wa maisha na namna mojawapo ya kuendeleza usemi wa kisiasa na kijamii (Hanks, 1989). Mimu kama rasilmali ya jamii zimefafanuliwa katika makala hii kwa kuchanganua dhima ya mimu katika jamii husika. Isitoshe, mimu kama matini huchanganuliwa kwa kuzingatia dhana ya mwingiliano wa matini ambapo matukio mawili yanaweza kukutanishwa katika mimu moja kupitia kwa maneno au picha. Suala hili limengaziwa katika sehemu ya uchaganuzi diskosi wa baadhi ya mimu zilizoteuliwa. Mwingiliano wa mitandao huwezeshwa na vyombo vya teknolojia ya mawasiliano hususan simu tamba. Katika mawasiliano ya simu tamba ujumbe mmoja huweza kutumwa katika mitandao ya *Facebook, Whatsapp, Twitter* na *Instagram* na mtu mmoja kwa wakati mmoja na huchukua muda mfupi sana kusambaa. Hili hufanikishwa zaidi na uwezekano wa mtu binafsi kuwa na maelfu ya wafuasi katika mitandao tofauti ya kijamii.

Wachanganuzi usemi kama vile Fairclough (2003), Tracy (2001) na Wodak na Meyer (2009a) wanaeleza kuwa maingiliano ya kijamii katika matini hueleweka matini hiyo inapochanganuliwa katika kiwango cha kauli na sentensi. Matini za kijamii kama vile mimu basi zinakuwa kama uzi unaounganisha mawasiliano ya kimakro na yale ya kimaikro. Yaani hubainisha jinsi lugha inavyotumika katika makundi makubwa ya kijamii (kimakro) na jinsi mtu binafsi au kundi ndogo la wanajamii mahsusi wanavyotumia lugha (kimaikro). Kwa hivyo, mimu humiliki sifa za matumizi ya lugha kitaifa na kimakundi kama vile sajili. Lugha inayotumika katika mimu hudhihirisha vipengele vya imani, itikadi na falsafa za jamii pana na za makundi maalum ya kijamii. Kwa mfano, imani za kishirikina, dhana gande za kikabila (hili ni suala la kitaifa) na itikadi za kisiasa kama zinavyokuzwa na kuenezwa na wanasiasa wa mirengo tofauti kupitia kwa matumizi ya lugha hasa uteuzi wa msamiati.

**Kiunzi cha Kinadharia**

Nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Kilongo ya Fairclough (1995) imerejelewa katika kuchanganua masuala ya kijamii yanayochangia kuibuka kwa mimu hizi mtandaoni. Kadhalika, miundo ya matini katika mimu pamoja na sifa zinazotokana na miundo hiyo zinachanganuliwa. Katika makala hii mimu imechukuliwa kama usemi au diskosi maalum. Kulingana na nadharia ya Fairclough (keshatajwa), usemi huwa na majukumu matatu; kujenga uhusiano, kupitisha mawazo na kujitambulisha. Katika kuchanganua usemi huu matini (*text*) huchunguzwa pamoja na jinsi matini hiyo inavyoundwa, kupokelewa na kutumiwa (*discursive practice*) na hatimaye jinsi jamii pana invyohusishwa na usemi huo (*social practice*). Mambo hayo yote hutokea katika tukio husika la mawasiliano. Katika makala hii vipengele hivi vya diskosi vimeangaziwa baada ya kutambulisha mimu zilizoteuliwa na kuzipanga katika kategoria maalum za kimaudhui. Mimu zilizoteuliwa zimechanganuliwa kama matini.

**MBINU ZA UTAFITI**

Mbinu iliyotumika katika utafiti huu ni ile ya usanifu taadhira (*exploratory research design*) kwa vile bado matumizi na uundaji wa mimu haujatafitiwa sana hususan nchini Kenya. Utanzu wa mimu hutumika sana nchini Kenya kama nyenzo ya burudani pamoja na dhima nyingine za Kijamii. Kwa kuwa uundaji wa mimu hufanywa na wasanii mashuhuri pamoja na wananchi wa kawaida, mimu ziliochanganuliwa zilitokana na makundi hayo mawili.

**Uteuzi wa Sampuli**

Maelfu ya mimu huundwa na kusambazwa na Wakenya kila uchao kupitia kwa mitandao ya kijamii. Kwa sababu hii, mtafiti alitumia mbinu ya uteuzi wa sampuli wa kimaksudi kupata mimu zitakazochanganuliwa katika utafiti huu. Mimu zilizotumika katika makala hii zilikusanywa kwa kutumia simu ambapo mtafiti alirekodi mimu kutoka kwa vikundi anavyoshiriki vya WhatsApp na katika mtandao wa Facebook kwenye ukurasa wake pamoja na kurasa za wasanii binafsi. Mimu zilizoundwa kwa lugha ya Kiswahili au mchanganyiko wa Kiswahili na Kiingereza na ambazo ni za wakenya ziliteuliwa. Mara nyingi sio rahisi kutambua mwanzilishi wa mimu zinazoundwa na raia wa kawaida moja kwa moja. Hii ni kwa sababu mitandao inayotumika kusambaza mimu ni mingi na waliounda mimu hizi huenda walitumia simu janja na kusambaza katika mitandao hiyo bila kuweka nembo au alama ya kuwatambulisha. Kuna maelfu ya mimu zinazoundwa kila uchao humu nchini na hivyo haiwezekani kuchanganua mimu zote. Mimu hamsini (51) ziliteuliwa kwa kuwa zingetosha kutoa sifa kamili za mimu zinazoundwa nchini Kenya. Kwa ajili ya kuhifadhi muundo asilia wa mimu hasa michoro, rangi, picha na ishara za *emoji*, mtafiti alidondoa baadhi ya mimu hizo jinsi zilivyokuwa katika mitandao husika ya kijamii na kuzihifadhi katika diski kuu ili kuzirejelea wakati wa uchanganuzi.

Baadhi ya mimu zinazorejelewa katika makala hii ni zile zilizopata umaarufu zaidi kati ya mwaka wa 2016 na 2020 kulingana na mijadala kwenye mtandao. Kipindi hiki kilishuhudia ukuaji wa kasi ya utanzu huu katika fasihi dijitali ya Kikenya. Aidha mimu zilizopewa kipaumbele ni zile za Kiswahili na zile zenye lugha mchanganyiko kwa kuwa Wakenya wengi huchanganya lugha. Wasanii maarufu wanaohusika na uundaji wa mimu za mtandaoni kama vile

@ChurchillNdambuki, @MugabeQuotes, @Karismemes, @Kenyan, @Pundit, @Wanjikutheteacher na mimu kadhaa za Wakenya wa kawaida au "Wanjiku" kama wananchi wanavyojulikana nchini Kenya. Mimu hizi ni nyingi mno na haziwezi kuorodheshwa zote. Lengo kuu hapa ni kubainisha jinsi ubunifu huu wa kisanaa unavyojitokeza hasa katika matumizi ya lugha. Miongoni mwa mimu zilizochanganuliwa ni zile zenye mianzo na umbo maalum kama vile "mimi", "pesa kidogo…" "Alafu", "Mugabe", 'abnormaree" "karismemes", "Kenyan",na "Churchill quotes

**Uchanganuzi Wa Data**

Mimu zilizoteuliwa kwa ajili ya uchanganuzi zilipangwa kwa kurejelea Mbinu ya Uchanganuzi maudhui na kategoria za kimaudhui na kiisimu zilidhihirika. Kategoria hizi zilimwezesha mtafiti kupanga mimu kulingana na sifa za miundo (mimu 20), dhima katika jamii kama vile za kuelimisha(mimu 13), kukosoa(mimu 20), kuelekeza (mimu 18); kulingana na jinsi mimu zinavyozalishwa kama vile mimu asilia na mimu ambazo ni vimelea vya mimu nyinginezo (mimu 23); mimu zenye sifa ya kuchanganya ndimi (mimu 22), na mimu zenye sifa ya mwingiliano matini (mimu 10). Jumla ya mimu 51 zilichanganuliwa. Baadhi ya mimu hizo ziliingia katika kategoria zaidi ya moja. Katika sehemu zifuatazo, uchangauzi data umefanywa kulingana na maudhui yaliyomo katika kategoria hizi.

Matumizi ya mimu nchini Kenya hufuata matukio ya kijamii, kisiasa na hata kiuchumi. Jambo muhimu au linalochukuliwa kuwa na ushawishi fulani kisiasa, kijamii, kiutamaduni na hata kimaadili linapotukia nchini, wakenya huunda mimu kulijadili. Mimu hizi huhusu masuala ya siasa na utawala, ugomvi wa kinyumbani, mauaji ya raia, uhalifu, udhalimu wa viongozi, ufisadi, utovu wa maadili, ukosefu wa ajira, mahusiano ya kijinsia na mengineyo. Mimu zinazoundwa huelimisha, kukosoa, kupasha habari na kuburudisha wanajamii. Kuna watu wanaotambuliwa kama waundaji wa mimu kwenye mtandao na hivyo wanachukuliwa kama wasanii wa fasihi dijitali. Hata hivyo wakenya wa kawaida wameanza kuibuka na mimu wakati mwingine muda mfupi tu baada ya tukio fulani kushuhudiwa. Mathalani, Rais anapotoa hotuba, waundaji mimu wanaweza kuchukua kipengele fulani cha hotuba hiyo na kukifanyia utani mtandaoni kwa kuongeza picha tuli, sauti, video na maneno machache.

Kenya ni nchi yenye wingilugha lakini lugha kuu zinazotumika katika mawasiliano rasmi na ya kawaida ni Kiswahili na Kiingereza. Lugha msimu ya Sheng' hutumika kwa wingi na vijana hasa maeneo ya mijini, jambo ambalo linajitokeza pia katika mitandao ya kijamii. Mawasiliano miongoni mwa Wakenya kwenye mitandao hii ya kijamii aghalabu huhusu masuala yenye mvuto yanayotukia kila siku nchini. Mengi ya masuala haya huwa yamewasilishwa katika stesheni za redio, televisheni na magazeti ya kitaifa. Wanahabari katika vyombo hivi vya habari huingiliana na hadhira wao katika mawasiliano na mijadala kwenye mitandao ya kijamii kama Facebook, Instagram na Twitter. Wananchi hutoa maoni yao katika mitandao hii ya kijamii na hivyo kushiriki katika mijadala na uchanganuzi wa pamoja wa masuala hayo. Wakati mwingine wahusika wa mijadala hii huuunda vichekesho ambavyo makala hii imevipa jina mimu. Kwa hivyo asilimia kubwa ya mimu zinazoundwa na wakenya huhusu masuala mazito au matukio ya kawaida ya

kijamii yanayotangazwa au kujadiliwa katika taarifa za habari zinazowasilishwa katika midia anuwai.

Mimu zinaweza kuwahusu wanasiasa, wafanyi biashara, watu wa kawaida kijijini au mijini, watoto na kadhalika. Kwa mfano, kuna mimu nyingi kuhusu wasichana wanaohudumu katika maduka ya Mpesa ambapo wanasawiriwa kama wenye kiburi na mtazamo hasi kwa wateja. Kadhalika, maelfu ya mimu kuhusu maisha ya kila siku ya wanajamii mashambani au mijini huibuka kila uchao katika mitandao. Kwa mfano, kuna mimu za *Our African mums* na *How mums teach*, ambazo zinazungumzia jinsi akina mama wa kiafrika huwapa nidhamu watoto wao. Maudhui haya ya kimsingi hutumiwa kuunda mimu nyingi ambazo zimeongezewa picha na maneno na hata video za aina tofauti tofauti huku zikidumisha maudhui hayo ya kimsingi. Misingi ya nadharia ya Fairclough (1995) imetumiwa kuchanganua mimu kama matini au aina ya diskosi yenye dhima maalum katika jamii ya Wakenya. Mifano maalum ya mimu na dhima zinazotekelezwa na mimu hizo katika jamii imetolewa. Ikumbukwe kuwa mada katika mimu zinaweza kutokana na visa vya kweli au zikawa ni za kiubunifu tu kama ilivyo katika utanzu mwingine wowote wa fasihi.

Nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Kilongo ya Fairclough, 1995 inarejelewa katika uchanganuzi wa mimu za Kikenya. Nadharia hii iliteuliwa kwa kuwa inahusu uhusiano baina ya matumizi ya lugha na miktadha ya kijamii. Kulingana na Fairclough na Wodak (1997), nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Kilongo haihusiki tu na miundo ya kijamii na kitamaduni bali huzingatia sifa za matini katika uchanganuzi wake. Katika nadharia hii, usemi au diskosi huchanganuliwa katika viwango vitatu. Kwanza ni kiwango cha matini, ambapo ujumbe wenyewe huchunguzwa kwa kuzingatia vipengele vya kiisimu. Uchanganuzi wa kiisimu unahusu uchunguzi wa vipengele kama uteuzi wa msamiati, mpangilio wa maneno katika usemi na maana inayotokana na mpangilio huo (Machin na Mayr, 2012). Kiwango cha pili ni utendaji diskosi (*discursive practice)* ambacho huhusu jinsi matini zinavyoundwa, kupokelewa na kutumiwa katika jamii. Katika kiwango hiki uchanganuzi wa matini unahusu uundaji, uandishi, mazungumzo, usomaji, usikilizaji na upokeaji wa matini. Kiwango cha matini na kile cha uundaji na utumiaji wake huelekezwa na kiwango cha tatu ambacho ni muktadha mpana wa jamii inayounda matini hizi (Fairclough, 2000). Katika makala hii mimu zimechanganuliwa kama matini zenye sifa za kimuundo na ambazo zina matumizi maalum ya kijamii kama inavyodhihirika katika sehemu zifuatazo.

**Uchanganuzi Mimu Kama Matini**

Dhana ya matini katika nadharia hii ya Fairclough (1995) hurejelea kumbukumbu ya matukio ya mawasiliano ambapo jambo fulani liliweza kuzungumziwa na kujadiliwa na wahusika fulani. Matini huweza kudhihirisha imani na uhalisia wa maisha ya wahusika katika mawasiliano. Kupitia kwa matini zinazoundwa katika jamii tunaweza kuongeza au kubadilisha maarifa, imani, mitazamo na hata desturi zetu (Fairclough, 1995). Katika utafiti huu matini ni mimu zinazoundwa na Wakenya kufuatia matukio tofauti katika jamii yao. Mimu hizi huundwa katika miktadha maalum na huenea haraka kupitia kwa mitandao ya kijamii. Kwa kurejelea sifa za kiisimu za matini hizi, data ya mimu zilizokusanywa ilionyesha kuwa mimu huwa na sifa maalum ambazo hufuatwa na takribani waundaji wote wa mimu hizo.

Kwanza, baadhi ya mimu zilizoundwa na Wakenya hudhihirisha sifa ya *uradidi* ambapo neno moja linaweza kurudiwa mara kadhaa katika matini moja. Kwa mfano, neno 'mimi' katika mimu zilizohusisha neno hilo kwa lengo la kuburudishana na kuelimishana.

Kwa mfano:

Mimu 1: *Mimi nilikwambia napenda madem wanavaa kamiisi, mimi?*

Mimu 2*: Kidogo kidogo utasikia madem wa Kenya wakisema hawakubali wanaume bila form tharee four bee.*

Mimu hizi zinazotumia maneno *mimi* na *kidogo kidogo* ni nyingi mno. Sifa hii ya uradidi huelekeza wanaounda mimu za kategoria hii. Pia mimu zingine zilitumia maneno kama *tibim, saitani, tialala* hata kama hazikuwa za kisiasa ingawa asili ya msamiati huu ni usemi wa kisiasa wakati wa kampeni za uchaguzi.

Sifa ya pili ya mimu ni *uundaji upya (reconstruction and mutation).* Sifa hii inahusu kutumia mtindo teule ambao tayari unatumika katika mawasiliano ya jamii kuibuka na mimu mpya. Mimu zinazotokana na hali hii huwa ni vimelea vya mimu nyinginezo zilizo na umaarufu zaidi katika jamii. Kwa mfano mimu ya *Salt bae* ilitokana na mpishi maarufu, Nusret Gokce aliyetuma picha yake katika mtandao wa *Instagram* ambapo anamimina chumvi kwenye nyama aliyokuwa akipika kwa majitapo. Kutokana tabia yake wanawake kwenye mtandao wakambandika jina '*Salt Bae'*. Kutokana na tukio hilo mimu za '*bae*' zilianza kuundwa mara kwa mara na Wakenya hususan kurejelea watu, vitu au hali zinazovutia. Kwa mfano, *Chilobae, Githeri is bae* na *Avocado is bae.* Pia ule umininaji wa chumvi ulitumiwa upya katika mimu kumhusu mwimbaji maarufu JayZ aliyeonekana kwenye mimu akimimina watoto wachanga. Jayz alikuwa ametangaza kuwa bibi yake alitarajia kujifungua mapacha na kutokana na hilo mimu zilizodhihirisha hali ya 'kumimina watoto' ziliundwa.

Mfano mwingine ni ule wa mimu zinazotumia mzizi wa "pesa kidogo"

Mimu: *Pesa kidogo ushaanza kuita sukuma greens na matatu public transport.*

Tatu, mimu huwa na sifa ya kuchanganya na kubadili msimbo. Asilimia kubwa ya mimu zinazoundwa na Wakenya hutumia lugha za Kiswahili na Kiingereza. Wakenya wana mazoea ya kuchanganya lugha ya Kiingereza na Kiswahili hata katika mawasiliano rasmi. Mtindo huu wa matumizi ya lugha umekuwa kama njia moja ya kujitambulisha kama Mkenya (kwa kiingereza *Kenyan Lingo*). Kulingana na Munuku (2005), lugha hizi huwa na dhima, hadhi na majukumu maalum nchini Kenya. Kwa mfano, lugha ya Kiingereza ina hadhi ya juu na ina nguvu kisiasa na kijamii pamoja na kuonekana kuwa ya kifahari kuliko lugha ya Kiswahili. Isitoshe, Wakenya wengi huitumia kwa uangalifu zaidi kuliko lugha ya Kiswahili huku wakijiepusha na makosa ya kisarufi au kimatamshi. Hata hivyo, Munuku (keshatajwa) akimnukuu Mesthrie (2000) anasema, lugha za Kiingereza na Kiswahili aghalabu huwa katika ushindani kimatumizi. Ingawa lugha ya Kiingereza ina hadhi na wengi huionea fahari, inachukiwa na baadhi ya watu wa tabaka la chini ambao hupendelea kuitumia lugha ya Kiswahili kutoa mawazo yao hasa kuhusiana na ukandamizaji unaotekelezwa na tabaka la juu dhidi yao.

International Journal of Linguistics

ISSN 2710-4788 (online)

Vol.3, Issue 1. No.3. pp 30 - 49, 2022

www.iprjb.org

Kutokana na hali hii ya mwingiliano wa lugha nchini Kenya, Wakenya wengi hupendelea kutumia lugha mchangayiko au lugha msimu ya Sheng katika baadhi ya mimu za Wakenya. Munuku (2005) anasema Wakenya wa tabaka la chini hasa vijana wanaoishi katika mitaa ya mabanda hupendelea Sheng kama chaguo lao asilia na hutumia Kiswahili na Kiingereza iwapo wanahitaji kuwasiliana na watu walio nje ya kikundi chao maalum. Kwa hivyo, Sheng inaweza kuchukuliwa kama msimbo wa kikundi maalum kilichojitenga na vikundi vingine katika jamii.

Mara nyingi Wakenya watachanganya lugha hizi katika mimu wanazounda na kuzisambaza vile vile katika mtandao kama njia moja ya kujitenga na jamii zingine au mataifa mengine mtandaoni. Kwa hivyo, mimu za Kikenya zinaibuka kuwa na msimbo wa kipekee. Aghalabu, katika mimu za Kikenya, lugha moja itatumiwa kudokeza na ya pili itatoa jibu. Kwa mfano, wakati wa uchaguzi wa 2017, kulikuwa na mimu iliyovuma sana:

Mimu: *The new line men are using kuingiza wanawake box (picha)* <u>*Vile kuko na tension ya elections hivi, si ukuje kwangu urudi baada ya uchaguzi?*</u>

Vinginevyo, baadhi ya mimu huwa ni mkusanyiko wa lugha kadhaa zikiwemo lugha za kiasili kama vile Gikuyu, Kikamba, Kidholuo, na kadhalika. Kuchanganya msimbo huwa na dhima fulani katika mawasiliano kama anavyoeleza Munuku (2005). Kwa mfano, watu huchangaya msimbo ili kutoa habari za ziada katika usemi. Uamilifu huu huonekana wakati mtumiaji lugha anadokeza usemi kwa lugha moja na kutoa jibu kwa lugha ya pili katika mimu. Mifano:

Mimu 1: "*Disciples were like: 'we ngai ma ya ngai!"*

Mimu 2: "*Hii Pombe ya kukunywa bila Tension sio tamu! We want lockdown back*!!!!!!

Kuchanganya msimbo pia huweza kuwa na dhima ya kubainisha hisia za msemaji, kudhihirisha mtazamo wa msemaji kuhusu lugha au mada husika, kufanya utani, kuchekesha, kufanya mchezo wa maneno na kadhalika. Haya yote hudhihirika katika mimu tofauti zinazoundwa na wakenya.

Sifa ya nne ya mimu ni <u>matumizi ya picha, michoro na maneno</u>. Mimu nyingi huwa na matini zenye mkusanyiko wa picha na maneno machache. Kuna mazoea ya kutumia ishara zinazotumika kwa wingi katika mitandao ya Kijamii, almaarufu kama 'emojis', katika mimu. Wakati mwingine, picha pekee ndizo zinazotumiwa kuunda mimu baada ya mimu ya kwanza inayoeleza picha hizo kutumika mtandaoni na kueleweka na wengi. Kwa mfano, mimu za matunda ziliweza kuundwa kwa wingi baada ya maelezo ya maana ya matunda hayo. Baada ya kutumika kwa muda, waundaji mimu walianza kuunda mimu za picha ya tunda tu bila maelezo yoyote. Mtu anaweza kutuma picha ya ndizi au nanasi pekee. Ishara hiyo ina ujumbe fulani wa mahusiano ya kimapenzi na hueleweka na wapokeaji lengwa wa mimu husika.

Tano, mimu huwa na sifa ya <u>kufinyanga sarufi</u>. Hapa mpangilio wa kawaida wa maneno katika sentensi hukiukwa na sentensi huenda ikakosa kukamilika. Kwa mfano katika mimu zifuatazo, sentensi inaonekana kama inayofuata maelezo yaliyotangulia lakini hayajatajwa. Si kawaida kuanza sentensi kwa neno 'halafu':

Mimu 1: *Alafu mtu anainsist unakuja lini Nairobi? Nothing against the city but it's a common line….*

Mimu 2: *Alafu Chebukati after hiyo time yote anasema I'm required by law to read the results in Kiswahili...acha niende hivi nacome.*

Mimu 3: *Alafu butter was for the rich.*

Lugha ya mtandao mara nyingi hukiuka kanuni za kisarufi hasa katika miundo ya sentensi na maneno (Batul, 2009). Kwa kuwa mimu ni sanaa ya mtandaoni, huwa mara nyingi inafuata mtindo huu wa matumizi ya lugha ya mtandao (*internet lingo).* Mathalan, kuna sifa ya matumizi ya vifupisho au akronimi katika mimu nyingi kama inavyodhihirika hapa: *LoL (laugh out loud), btw (by the way), plz (please) 21002 (tumia tu), tx (thanks), k (okay).*

Sita, mimu nyingi zilizoundwa na Wakenya zina sifa ya msamiati teule katika mundo wake. Jambo hili huonekana zaidi katika maneno yanayojitokeza kwa njia spesheli kutokana na matumizi yake nchini Kenya. Usanifu wa maneno hayo huwa umevurugwa kimaksudi. Mifano ya maneno hayo ni kama *okei, saitani, isorait* ambayo yametumika katika mimu nyingi sana.

Sifa ya saba ni matumizi ya maneno na picha zilizoteuliwa katika mimu zinazodhamiriwa kuibua hisia tofauti kama vile huzuni, hasira, furaha, mshangao na hisia mchanganyiko. Mathalani, ishara za emoji (picha zinazochorwa kwa kutumia zanaviolwa maalum mtandaoni) hutumika kuwasilisha hisia hizi. , Picha halisi za watu pia hutumika kubainisha hisia maalum. Kwa mfano Wakenya wengi hutumia picha za wanasiasa kama vile Rais Uhuru Kenyatta kuonyesha hisia za furaha, bezo, kejeli, dharau au hasira. Picha ya Michael Jordan akitiririkwa na machozi hutumika na Wakenya kubainisha hisia za uchungu na majonzi.

**Uchanganuzi wa Utendaji diskosi**

Kiwango cha utendaji diskosi kinahusu uundaji, upokezi na ufasiri wa usemi ambao katika makala hii ni mimu zinazoundwa na Wakenya. Mchakato wa kuunda mimu hufuata mkondo maalum. Muundaji anaweza kutumia malighafi kama vile *KnowYourMemes.com* na *memecreators.com* ambayo tayari yapo kwenye mtandao kuchanganya picha kisha akaongeza maneno na ishara maalum (Chandler, 2013). Mara nyingi mimu za mtandaoni huundwa na watu mashuhuri hasa wanakomedia na wafanyikazi katika sekta ya uanahabari na vile vile raia wa kawaida. Mimu hizi zinapoundwa na mtu mmoja huenea kwa haraka na huendelea kuundwa upya katika mpito wa wakati. Kuna watu au makundi yaliyoibuka kwenye mtandao ambao kazi yao kuu ni kuunda mimu na hupata riziki kutokana na wafuasi wengi au idadi ya watu watakaozifuatilia mimu zao. Nchini Kenya kuna waundaji mimu mashuhuri kama vile Kariuki (@karismemes), Daniel Churchill Ndambuki na Wanjiku the Teacher wenye wafuasi wengi mtandaoni. Watu wa kawaida huibuka na mimu kisha zinaenea lakini sio kwa haraka kama wasnii wanaofahamika na wenye umaarufu au ushawishi mkubwa kwa umma.

Upokezi wa mimu hutegemea mambo kama vile lugha iliyotumika (mimu za Kiswahili au lugha mchanganyiko huenea haraka zaidi kuliko zile za Kiingereza pekee), maudhui yake (ikiwa inahusu wakenya itaenea zaidi) na mwanzilishi wake. Lugha ya Kiswahili ni lugha ya walio wengi nchini Kenya na kwa hivyo mimu zinapotumia lugha hii hupokelewa na kukubalika kwa urahisi zaidi. Maudhui ni kipengele muhimu sana katika mimu. Mimu zinazohusu masuala yanayomkumba Mkenya wa kawaida zinasambazwa kwa kasi zaidi ya mimu zinazohusu masuala ya kigeni au

tabaka la juu. Mwanzilishi wa mimu huwa ni kipengele muhimu katika kuenea au kufa kwa mimu hiyo. Mara nyingi vijana ndio wanaounda mimu hizi na huzieneza haraka kwa vile ndio wanaotumia mitandao ya kijamii kwa wingi zaidi kupitia kwa simu janja. Mimu zinazoundwa huweza kuonyesha jina la msanii au la, na hilo huathiri kusambaa kwake pia. Kwa mfano, msanii maarufu wa mimu anayejulikana kwa jina la mtandao @Karismemes ameunda mimu nyingi ambazo mara nyingi hutokana na masuala ibuka katika jamii. Kwa kuwa msanii huyu anafahamika na watu wengi, mimu zake huwa zinasambaa haraka. Hata hivyo, mimu zinapopitishwa katika mitandao ya kijamii hazihitaji kutambulisha muundaji wake bora tu watumiaji wanaweza kuelewa muktadha wa matumizi. Kwa mfano, mimu zinazohusu masuala ya kisiasa yaliyoudhi au kufurahisha jamii zitaenea hata iwapo msanii aliyeziunda hajulikani. Aidha, mimu huundwa na kusambazwa katika kiwango cha kimaikro lakini athari zake ni za kimakro (Knobel na Lankshear, 2007). Hili linamaanisha kuwa mimu Zinaweza kuundwa na mtu mmoja pengine kwa nia ya burudani tu lakini athari zake zikawa nyingi na zikagusa jamii pana zaidi. Kwa mfano, mimu za *githeri man* zilizoundwa wakati wa kupiga kura nchini Kenya, zilienea haraka na zikawa na athari za kitaifa na kimataifa.

**Uchanganuzi wa Matumizi ya Mimu katika Kiwango cha Jamii**

Kiwango cha tatu cha Uchanganuzi Diskosi Hakiki ni utendaji halisi wa jamii. Lugha huwa imekamilika inapotumika katika miktadha anuwai ya kijamii kutimiza mahitaji ya jamii kimawasiliano. Kama ilivyotajwa awali, mimu huundwa kutokana na matukio katika maisha ya kila siku ya wanajamii husika. Uundaji wa mimu huwa umeafiki kanuni hii ya kipragmatiki kwani mengi yanayotukia katika jamii fulani, hutumika kama malighafi ya kuunda mimu. Kupitia kwa mimu watu huweza kufanyiana utani, kutoa maoni na kubainisha hisia tofauti na kadhalika (Baukhage, 2011). Mimu zote zilizokusanywa zilibainisha kuwa hakuna mimu inayotokea tu ghafla bila kuhusishwa na suala au tukio fulani katika jamii husika. Masuala ya kisiasa kama vile mikutano ya hadhara ya wanasiasa, ajali, vituko vya kidini, kampeni za kisiasa, mahusiano ya kijinsia na yale ambayo huripotiwa katika vyombo vya habari huchangia katika kuibuka kwa mimu hizi. Kwa mfano mimu zenye mwanzo "Mimi" zilitokea baada ya Rais Uhuru Kenyatta kumwambia Gavana wa jiji la Mombasa, Hassan Joho, kuwa hafai kumfuata kwa kuwa si bibi yake. Maneno aliyotamka ni: "*Mimi si bibi yake....*"

Matumizi ya lugha katika jamii yanafaa kulinda na kudumisha maadili ya jamii husika pamoja na mila na desturi zake. Hata hivyo baadhi ya mimu hukiuka sheria hii kwa kuwa utovu wa adabu unadhihirika kupitia kwa msamiati ulioteuliwa. Baadhi ya mimu hizi hutumia maneno ambayo kawaida huwa mwiko kutumia moja kwa moja katika lugha ya Kiswahili hasa kuhusiana na suala la ngono. Mifano hii haiwezi kutolewa katika makala hii kwa sababu za kimaadili lakini ipo katika mitandao ya kijamii.

Maneno yanayotumika kwenye baadhi ya mimu za mtandaoni ni yale yanayoeleweka wazi kietimolojia na mara nyingi hufahamika katika jamii pana. Kuelewa nyingi za mimu hizi huhitaji mtumiaji kuelewa muktadha wa matumizi yazo kijamii. Kwa mfano mimu zenye maneno teule kama *mimi*, *bae, alafu*, *githeri*, *kidogo kidogo, canaan, tibim* na *supreme coat.*

Vilevile, baadhi ya mimu zinazoundwa na Wakenya huhusisha visa muhimu vya kijamii na watu mashuhuri katika jamii. Kuna mimu nyingi za kisiasa zinazohusu utawala, viongozi wa kaunti, rais, wabunge, mawakili na kadhalika. Kwa mfano kuna mimu inayokosoa wanawake ambao hutegemea usaidizi wa wanaume, kisha inaambatishwa picha ya Raisi Kenyatta ikikaa kama ndiye anayeuliza swali hilo:

Mimu: *Alafu kuna hawa wasichana wanatoboa kila kitu! Mara ulimi mara eyebrows mara mapua mara mukonyo. Jameni…na maisha mtatoboa lini.*

Mimu pia hutumia maudhui ya siasa na ya kijamii kama malighafi. Mengi ya maudhui haya huonyesha imani, mila na desturi za Wakenya kwa jumla. Mimu kama zile zinazoonyesha imani na desturi kuhusu makabila tofauti nchini, uwe ukweli au la hudhihirisha hali hii. Kwa mfano:

Mimu 1: *Mimi Nyambura nikasema napenda supu nyingi mimi?.*

Mimu 2: *Mimi nilisema siwezi kula pizza bila soup mimi?.*

Mimu hizi zimejengwa kwa misingi ya dhana gande kuwa wanawake wa jamii ya Wakikuyu hawajui upishi.

**Dhima ya Mimu katika jamii**

Mimu zina dhima kubwa katika jamii kama utanzu mwingine wowote wa fasihi. Jamii ya sasa hutegemea sana TEHAMA na mawasiliano ya mtandaoni zikiwemo mimu. Mimu hupata umuhimu kutokana na majukumu yake katika jamii kwa jumla. Kwa mfano, Chandler (2013), anasema mimu zinaweza kutumika kama njia ya kupinga unyanyasaji wa tabaka tawala katika jamii kupitia mawasiliano yanayotokea nje ya miundo msingi yenye nguvu za kisiasa na za kijamii. Hata katika kampeni za kisiasa za mwaka wa 2020 mimu ziliibuka kuwa zana muhimu za kuwavutia wapigaji kura katika nchi zilizokuwa na uchaguzi. Kwa mfano, mwaniaji kiti cha Urais cha Marekani, Michael Bloomberg, aliwafadhili wafuasi takribani milioni 60 katika mtandao wa *Instagram* ili waweze kuunda mimu kuhusiano na kampeni yake. Hatua hii ilizua mjadala mkali na upinzani kutokana na kile kilichochukuliwa kama kuuchukulia uundaji mimu kama matangazo ya kisiasa au kitu kinachoweza kulipiwa au kununuliwa.

Mimu nyingi zinazoundwa na Wakenya huhusu matukio ya kisiasa na kijamii. Kinachofanyika katika mikutano ya kisiasa hasa katika kampeni za uchaguzi au wakati wapinzani wanapoikosoa serikali hupelekea wasanii wengi kuunda mimu zinazoeleza au kukosoa matukio hayo kwa njia ya utani. Jumbe zinazowekwa katika mimu hizi hata hivyo hurejelea masuala mazito ya Kijamii hususan ya kimaadili. Kwa mfano, panapokuwa na kashfa ya ufisadi kama wizi serikalini au matumizi mabaya ya mamlaka na nguvu, mimu huundwa kukosoa tabia hizi za wanasiasa. Wanasiasa huweza kutumia mimu kufanya kampeni za kisiasa. Mimu husaidia wanajamii kujiepusha na vikwazo vinavyokumba vyombo vya habari vya kawaida na kukosoa, kukashifu na kukejeli mifumo dhalimu ya unyanyasaji.

Mimu hutumiwa pia kuburudisha wanajamii katika mitandao ya kijamii kupitia kwa picha za kuchekesha pamoja na maneno ya ucheshi na mzaha. Kwa hakika asilimia kubwa ya mimu zina dhima ya burudani tu. Kwa mfano mimu kama: "*Venye madem wakale huruka*". Maneno haya

yanafuatwa na picha ya msichana mwenye miguu mirefu akiruka ukuta mrefu kuonyesha kuwa jamii hiyo ina wanariadha maarufu wake kwa waume. Mifano mingine:

Mimu: "*Niwaulize? Hata sisi wenye tunafunzwa na ulimwengu tunarudia next year...?*

Pia mimu nyingine yenye dhima ya kuburudisha tu ni:

Njoro: *Mimi pia ni foodie*

Me: *So unapenda kukula kula*?

Njoro: *Hapana mimi ni foodie wa viatu*

Me*: ?* (Ikiandamana na picha ya mtu anayecheka kwa dharau)

Mimu: (picha ya Rais Kenyatta kando ya bahari) "*Ningeingia kuswim but NTV watareport, 'Uhuru ako maji'*

Mimu: "*Mbona leo kuna weather ya KCSE*" Mimu hii iliundwa wakati wa baridi kali. Watu wengi huogopa mtihani wa kidato cha nne, almaarufu KCSE, kwa kuwa ndio unaoamua utakavyoendelea maishani. Mimu zingine zilizoundwa wakati wa msimu huo ni kama:

*Cold season chapter 1 verse 5 says...*"*He who has looked at the soap and water has already bathed*"

Jukumu lingine la mimu ni kukashifu utovu wa maadili katika jamii. Mimu hufunza maadili ya jamii na kuikosoa jamii inapovuka mipaka. Kwa mfano, mimu hukashifu tabia kama ukahaba, uzini, ukosefu wa uaminifu na utovu wa adabu kwa jumla. Mimu hizi ni nyingi na zinaibua wazo kuwa jamii inajikosoa kupitia kwa utanzu huu. Mimu hutumiwa pia kuzindua wanajamii kuhusu matukio tofauti ulimwenguni kama vile uchaguzi, mitindo ya mavazi, uchumba, malezi, siasa, magonjwa na mengineyo. Kwa mfano, mimu yenye picha ya maembe mengi yaliyoumwa ambayo huandamana na maneno: *Kenyan men when looking for wife material. Saitani!* Maneno haya yanakashifu tabia ya wanaume kushiriki katika uhusiano wa kingono na wasichana wengi huku wakiwaacha taabani mara kwa mara kutokana na tamaa ya mapenzi. Katika mimu hii ujumbe ni kuwa maembe yaliyoumwaumwa hayawezi kutamanika tena, ishara ya jinsi maisha ya wasichana hawa yanavyoharibiwa na wanaume wenye tabia za kikware au vinginevyo kipaka shume. Mimu nyingine ya kimaadili ni kama ifuatayo hapa chini:

"*Dame mrembo sana*

*akiolewa na mzee rika ya babake,*

*tunaeza muita msichana marrydaddy*"

Mimu kama hii inakosoa tabia za wazee wenye familia zao kukiuka maadili ya ndoa na kushiriki kimapenzi na wasichana wadogo wa rika la watoto wao.

Kwa upande mwingine mimu zinaweza kuchangia katika kuporomoka kwa maadili ya wanajamii. Mathalan, baadhi ya mimu hutumia lugha chafu na pujufu kama njia ya kuburudisha wanajamii lakini hiki ni kinyume cha kanuni za kimaadili za jamii nyingi hasa za Kiafrika.

Mifano ya mimu kama hizi ni:

International Journal of Linguistics

ISSN 2710-4788 (online)

Vol.3, Issue 1. No.3. pp 30 - 49, 2022

www.iprjb.org

"*Asubui huwa*

*unaamshwa na*

*kiss forehead ama*

*unatingishwa kama*

*syrup ya minyoo*?"

Mimu nyingine inayoenda kinyume na maadili ni:

"*Sio kila ndoa huanza na*

*"will you marry me?"*

*Zingine zilianza na*

*"Baba amesema nirudi mahali nilipolala"*

Katika mifano hii kuporomoka kwa maadili miongoni mwa vijana kunadhihirika kupitia kwa mahusiano ya kimapenzi kabla ya ndoa. Hili linajitokeza pia katika meme kama " *Halafu mkioga na maji ya mvua jipake marashi priss; nimehug kadame kengine kananuka mabati"* Mimu kama hii japo ina mafunzo kwa jamii kama vile kudumisha usafi, bado inaporomosha maadili kwa kuwasawiri wanawake kama chombo cha burudani tu.

Baadhi ya mimu hudumisha dhana gande ambazo ni mambo yasiyo na mashiko yanayohusishwa na kabila au kikundi fulani cha watu katika nchi au jamii pana. Dhana gande huzuia utangamano wa wanajamii hasa zinapokuwa hasi. Kuna mimu zinazorejelea dhana kuhusu sifa zinazohusishwa na jamii fulani na ambazo hufanya jamii kama hiyo kuchukiwa. Kwa mfano, kuwa watu wa kabila fulani ni wezi, wengine walafi, wengine wachafu, wengine wachawi na kadhalika. Mimu hizi huonekana kama zenye lengo la kuburudisha lakini ukweli ni kuwa zinaweza kushindilia mitazamo hasi kuhusiana na mahusiano ya kijamii. Kwa mfano:

Mimu: "*Leo tuligombana na jirani yangu kuhusu kuibiwa kwa redio yake. Sasa nasikia amesafiri kwenda kitui. Is that how neighbours solve issues, surely?"*

Mimu hii inaashiria kwa njia fiche kuwa kuna jamii fulani inayoaminika kushiriki uchawi na ushirikina. Kwa hivyo kanado na kuburudisha wanajamii mimu hii inaunga mkono dhana gande hasi ya ukabila na unyanyapaa dhidi ya jamii husika.

Nchini Kenya mimu zimeweza kutumiwa kibiashara kama vile katika kutangaza bidhaa za kampuni tofauti. Kwa mfano, kampuni ya mawasiliano ya Safaricom na benki ya Kenya Commercial Bank hutumia mimu kutoa taarifa za kibiashara kwa wateja wao.

Mimu 1: Safaricom: *Sisi mnasema tunakulanga bundles sisi?*

Mteja mmoja wa Safaricom pia akajibu: *Mimi? Mnasema niko na deni yenu ya Mshwari? Mimi?*

Mimu 2: KCB: *Sisi? Tukasema uchukue loan na usilipe? Sisi?*

Mteja: *Mimi? Nikasema shamba yangu ni collateral? Mimi?*

Kadhalika, mimu huweza kuchangia katika kujenga utangamano wa wanajamii hasa kwenye mtandao. Kwa mfano, wakati janga la virusi vya korona lilipozuka hasa mwanzoni mwa mwaka wa 2020, watu wengi waliingia mtandaoni ili kutangamana na marafiki ambao sasa hawangeonana nao uso kwa uso. Kupitia kwa mimu wengi walijiburudisha na kuondoa kiwewe na hofu waliyokuwa nayo. Ugonjwa wa virusi vya korona ulipozuka na serikali ikaweka sheria na mikakati ya kuzuia maenezi zaidi kama vile utengwaji, karantini na ujitengaji kulikuwa na mimu nyingi zilizorejelea hali mpya kama vile: "*Babe is ukuje self isolation kwangu; tutaweka social distancing.* Mimu zilizohusu jinsi ya kujikinga kutokana na virusi, njia mpya utendaji kazi kupitia mitandao kama *Zoom* na *Google Meet* pia zilizuka. Tabia za watu katika mikutano hii ikawa ni suala sio tu la burudani lakini la kukosoana na kuelimishana. Kwa mfano, Mimu iliyohusu njia mpya ya kukwepa shule au kazi:

Mimu 1: Mwalimu: *Joan, andika jibu la swali nililouliza na uweke video tuweze kukuona*

Joan: *Kitufe cha kifaa kilichozimwa au neno 'offline' linaonekana badala ya jibu*

Mimu 2: Kazini: Mtu anaestahili kuwa mkutanoni anaandika ujumbe:

*Tafadhali sikusikii hata kidogo, nadhani mtandao wangu una tatizo*

Picha inayowekwa kwenye mimu ni ya mtu aliyelala kisha ameshika simu ya rununu ambayo anatumia kuchezea michezo ya mtandaoni badala ya kuhudhuria mkutano. Mfano huu wa matumizi ya mimu unaonyesha dhima ya meme ni kukosoa utovu wa maadili ya kazi na kufichua yanayotendeka katika maisha halisi huku ikiburudisha wasomaji mimu.

Mimu 3: *Siku hizi sisi watu wa Forehead ndio kusema...wale wa dimples na mwanya zote ziko kwa mask...kila kitu kina wakati wake"*

Mimu 4*: April: "10 cases is too much. Kenya is about to become Italy"*

*July: "Ati 300 cases? Wah Crazy. Anyway Sato Kiambu ama Karen?" #NewNorma#DomesticTourism#HapaWithinTu.*

Mimu 4 ilidhamiria kuonyesha jinsi Wakenya wanapuuza kanuni za kujikinga kutokana na virusi vya korona. Inabainisha kuwa mwanzoni kesi zilipokuwa chache kulikuwa na uoga mwingi lakini kesi zilipokuwa zinaongezeka na hali kuzoeleka watu wakaanza mapuuza ya sheria mpya.

Mifano mwingine ni mimu zilizoundwa na wakenya katika kipindi hiki cha virusi vya korona baada ya wengi wao kupoteza ajira na njia za kujikimu. Mathalani:

Mimu: "*When is the next Bantu migration? Am fed up with Kenya (*picha ya bendera ya Kenya). *I miss Shungwaya* (ishara/emoji ya kilio).

Mfano mwingine wa mimu ni ile ya tunda iliyovuma sana mwaka wa 2017 na bado hurejelewa na baadhi ya watu mara kwa mara. Mimu hii ilihusu kutuma tunda linaloweza kueleza maisha yako kwenye mitandao ya kijamii. Pia ilitumika kufanya kampeni ya ulaji wa vyakula bora ili kudumisha afya nchini. Mimu hiyo pia ilitumika na kampuni ya Bonfire Adventures kutangaza biashara yao ya usafiri. Walitumia tunda la nazi kuashiria safari za kuelekea jiji la Mombasa.

International Journal of Linguistics

ISSN 2710-4788 (online)

Vol.3, Issue 1. No.3. pp 30 - 49, 2022

INTERNATIONAL PEER REVIEWED JOURNAL AND BOOK PUBLISHING

www.iprjb.org

Kwa kuwa wengi katika mtandao huogopa kujipata mashakani kisiasa, mimu hutumika kukosoa wanasiasa na wanajamii wenye mamlaka bila kujipata mashakani hasa kuhusiana na masuala kama ufisadi, ukosefu wa ajira, udhalimu wa polisi, mauaji ya raia, uhalifu, migomo na kadhalika. Mfano mzuri ni *meme* za *canaan* na *tibim* zilizohusu uchaguzi mkuu wa mwaka 2017 nchini Kenya.

Pia mimu kama: *BEES poliinate a flower, you pick the flower and give it to someone who calls you HONEY...Corruption starts with YOU.*

Mimu pia hudhihirisha migogoro ya kitabaka iliyopo katika jamii lengwa. Kuna mimu nyingi zinazoundwa na watu wa tabaka la chini kukosoa tabaka la juu na kuonyesha matatizo yanayowakumba wachochole nchini Kenya. Kwa mfano:

Mimu 1: *Mahali huu mwezi uko, naona nikinunua tropical za thirty bob nikuwe hawker nisilipe fare"*

Mimu 2: *Shida ya umaskini ni kuwa huwezi jua kama ni stima imepotea au ni token zimeisha"*

Mimu 3: *Imagine msee amebeba githeri siku moja ashakuwa celeb na wengine wamebeba guitar hadi mgongo umekuwa kama question mark na bado gigs ni tricky*"

Mimu 4: *When your mother in law says umsaidia kupika chapo but USIU taught you how to order pizza* (kisha kuna picha ya msichana aliyezirai)

Mimu 6: *Ile siku umesota hadi unaoga na sabuni ya vyombo kisha ukiingia kwa mat unasikia lighskin akiambia conda, "hii gari inanuka sufuria" (mimu hii ina picha ya Rais Kenyatta akicheka kwa nguvu*)

**Nafasi ya lugha ya Kiswahili katika Uundaji na Matumizi ya Mimu**

Mimu nyingi nchini Kenya huundwa kwa kutumia mchanganyiko wa lugha ya Kiingereza na Kiswahili. Mara nyingi lugha ya Kiswahili hutumika kwa kuwa inawafikia wengi. Hata hivyo, kama inavyodhihirika katika mifano iliyotolewa hapo juu, lugha inayotumika huwa ni ya mtaa ambayo mara nyingi hukiuka kanuni za kisarufi na hutiwa nakshi na lugha msimu ya sheng'. Mimu zimeweza kutumika katika diskosi za kitaifa kueleza masuala ibuka kwa njia ya utani lakini hata zinapotumika kwa kiwango hicho bado nyingi zina sifa ya kuchanganya msimbo. Hata hivyo, bado lugha ya Kiswahili inatumika kwa wingi katika mimu za Wakenya na hivyo kuendelea katika matumizi yake kama lugha ya taifa. Ingawa mimu ni utanzu usioweza kufungika katika mipaka ya kitaifa kwa kuwa mtandao ni sehemu ya utandawazi, mimu nchini Kenya huonekana kuwa na lengo la kuwafikia wakenya kutokana na lugha inayotumiwa ambayo huwa ya mchanganyiko na mada zinazozungumziwa. Takribani mimu 36 miongoni mwa zile 51 zilizorejelewa zilitumia lugha ya Kiswahili au mchanganyiko wa lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Aidha mimu nyingi (asilimia 86) zilionekana kutumia neno la Kiingereza kutokana na mazoea ya matumizi ya lugha hii katika jamii ya wakenya. Mimu nyingi huundwa na vijana, kati ya miaka 18 na miaka 35 kwa kuwa wanamiliki stadi za kutumia programu-tumizi na zanaviolwa maalum ambazo ndizo malighafi za kuunda mimu mtandaoni. Hivyo matumizi ya lugha mchanganyiko kuunda mimu ni suala la kawaida maana wengi hutumia lugha za Kiswahili na Kiingereza kwa njia isiyo sanifu

pamoja na Sheng'. Hata hivyo, tabia hii imedidimiza zaidi matumizi ya Kiswahili sanifu mtandaoni

## MATOKEO YA UTAFITI

Makala hii imeangazia sifa maalum za kijamii na kiisimu ambazo zinazitambulisha mimu kama utanzu wa kipekee wa fasihi dijitali. Uchanganuzi wa mimu teule umedhihirisha kuwa mimu zina muundo maalum kisarufi, ambao unaonekana kukiuka sheria za kisarufi za sentensi za kawaida. Pia imebainika kuwa nchini Kenya mimu nyingi hutumia mchanganyiko wa lugha ya Kiswahili (lugha ya mtaani) na Kiingereza ingawa kunazo zinazotumia Kiswahili pekee. Vijana nchini Kenya wana mazoea ya kubadili na kuchanganya lugha za Kiswahili na Kiingereza pamoja na Sheng'. Uundaji wa mimu mara huweza kufanywa na watu wanaotambulika katika jamii ya mtandao (jamii meme) kama wakuza mimu au watu wa kawaida wasiojulikana. Mimu zinapoundwa huenea kwa haraka na hubadilika katika mpito wa wakati kimuundo na kimsamiati. Aidha, dhima kadhaa za mimu katika jamii lengwa zimeweza kujadiliwa na ikadhihirika kuwa mimu ni utanzu wenye majukumu muhimu katika jamii pana. Imebainika pia kuwa matukio katika jamii huelekeza uundaji wa mimu na kwa hivyo mimu hutegemea miktadha tofauti ya mawasiliano ya wanajamii kimaudhui na kimatumizi. Aidha, imewekwa wazi kuwa zaidi ya burudani inayotokana na utani uliomo katika mimu hizi wanajamii huelimishana kuhusu masuala muhimu katika jamii yao. Mimu zinatumiwa kutetea haki za walio katika tabaka la chini na kukosoa tabaka tawala. Vilevile, jamii huweza kujikosoa na kujiadhibu yenyewe kupitia kwa mimu hizi. Aidha, mimu hizi zilionekana kuibuka mitandaoni au kuundwa kwa wingi kila mara palipotokea tukio muhimu katika jamii na hivyo kuwasaidia wanajamii kulielewa zaidi.

## HITIMISHO

Utanzu wa mimu unapaswa kuendelea kukuzwa na kufanyiwa utafiti. Mimu ni utanzu ambao umechangia katika kupanua nafasi ya kuendeleza demokrasia na haki ya walio wengi kusikika katika jamii kupitia kwa lugha yao. Kwa sababu hii, mimu ni utanzu ambao unahitaji kufanyiwa utafiti zaidi maana unaibua namna mpya ya kutumia lugha ikiwemo lugha ya Kiswahili na hivyo ina athari zake katika sarufi na matumizi ya lugha mchanganyiko. Mimu nyingi nchini Kenya huchanganya lugha za Kiswahili Kiingereza pamoja na lugha msimu ya Sheng' na lugha zingine za kiasili. Kwa kuwa mimu ni utanzu unaofikia wengi katika jamii, ni muhimu ukuzwe na kutumiwa ipasavyo na wanajamii. Kwa mfano, wataalamu, walimu na wasomi wa lugha ya Kiswahili wanaweza kuendeleza matumizi ya lugha safi na sanifu kupitia mimu zenye mianzo maalum. Kwa mfano, mimu zenye mianzo ya methali kama *mwenye*, *kilicho*, *cha* and kadhalika zinaweza kutumika kisha washiriki wakajaza pengo kwa kutumia methali halisi. Katika kufanya hivi mshiriki anaweza kukosolewa na kuelekezwa na wenzake. Lugha hatimaye itakuwa imelindwa kimatumizi na maadili ya jamii yatadumishwa. Kwa jumla, mimu ni utanzu unaoweza kutumika katika ufundishaji wa lugha ya Kiswahili kwa kutumia vifaa vya teknolojia ikiwemo simu na mtandao na haupaswi kupuuzwa.

**MAREJELEO**


Baukhage, C. (2011). Insight into Internet Memes. 5th International AAAI Conference on Weblogs and Social Media, Bonn, Germany.

Batul, F. (2009). *Chatspeak: Linguistic Evolution or Devolution.* New York: Pergamon Press.

Blackmore, S. (1999). *The Meme Machine.* New York: Oxford University Press.

Chandler, R. (2013). Meme World Syndrome: A Critical Discourse Analysis of the First World Problems and Third World Success Internet Memes. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Central Florida.

Chandler, D. and Munday, R. (2011). *A dictionary of Media and Communication.* New York: Oxford University Press.

Crystal, D. (2001). *Language and the Internet*. Cambridge: Cambridge University Press.

Ekdale, B. & Tully, M. (2014). Makmende Amerudi:Kenya's Collective Reimagining as a Meme of Aspiration. In, *Critical Studies in Media Communication* Vol. 31, 283-298.

Fairclough, N. (1995). *Critical Discourse Analysis: The Critical Study of Language.* Harlow: Longman.

Fairclough, N. and Wodak, R. (1997). Critical Discourse Analysis. In, Van Dijk (ed) *Discourse as Social Interaction.* London: SAGE Publications.

Fairclough, N. (2003). *Analyzing Discourse.* New York: Routledge.

Flecha Ortiz, J.A., Santos Corrada, M.A., Lopez, E. & Dones, V. (2021). Analysis of the Use of Memes as an Exponent of Collective Coping During COVID-19 in Puerto Rico. *Media International Australia,* 178(1), 168-181, https://doi.org/10.1777/1329878X20966379

Gelb, B.D. (1997). Creating 'Memes' While creating Advertising, *Journal of Adverising Research,* 37(6), 57-59.

Hanks, W.F. (1989). Text and Textuality, *Annual Review of Anthropology Journal.* Vol. 1895-127(Oct 1989)

Henry, R. (2019). Role of Artificial Intelligence in New Media (Technology Based Perspective), *CSI Communications,* 42(10): 23-25.

Iloh, C. (2021). Do it for Culture:The Case for Memes in Qualitative Research. In, *International Journal of Qualitative Methods, Vol. 20, 1-10.* https://doi.org/10.1177/16094069211025896

Jenkins, H. (2006). Confronting the Challenges of Participatory Culture: Media Education for the 21st Century. *White Paper, McArthur Foundation*, Chicago, Illinois.

Kulkarni, A. (2017). Internet Meme and Political Discourse: A Study on the Impact of Internet Meme as a Tool in Communicating Political Satire. *Journal of Content, Community and Communication,* Vol.6 Year 3, ISSN:2395-7514

Leong, P. (2015). Political Communication in Malaysia: A Study on Use of New Media in Politics. *Journal of Democracy-Creative Commons*

Locke, T. (2004). *Critical Discourse Analysis.* New York: Continuum.

Machin, D. and Mayr, A. (2012). *How to Do Critical Discourse Analysis.* Thousand Oaks, CA: SAGE.

Milner, R. (2012). The World Mode Meme: Discourse and Identity in Participatory Media. Tasnifu ya Uzamifu (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Kansas.

Mukongo, L.L. (2020). Participatory Media Cultures: Virality, Humour and Online Political Contestations in Kenya. In, *Africa Spectrum* 2020, Vol. 55(2) 148-169.

Munuku, A.W. (2005). Code Switching in the Contemporary Kiswahili Rap Song.Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Nabea, W. (2021). The Discursive Counter-Power of Internet Memes in Response to the Management of the COVID-19 Pandemic in Kenya. In, *English Academy Review* 38(2):117-134.

Rasheed, A.A.P.K. Maria, C. & Michael, A. (2020). Social Media and Meme Culture: A Study on the Impact of Internet Memes in Reference with 'Kudathai Murder Case'